




# Shughuli za Njoo, Unifuate

Kwa ajili ya jioni ya nyumbani, au kujifunza maandiko—au kwa ajili ya burudani tu!



Agosti 26–Septemba 1

## Misingi Thabiti

KWA AJILI YA HELAMANI 1–6

Helamani alifundisha wanawe kujenga maisha yao juu ya Mwamba imara wa Yesu Kristo (ona Helamani 5:12). Msingi ni kitu kile ambapo juu yake hujengwa kitu fulani. Msingi imara unafanya jengo zima kuwa imara, hata katika dhoruba. Jenga minara miwili—mmoja juu ya msingi imara na mmoja juu ya msingi dhaifu. Mnara gani ni thabiti zaidi? Ni kwa jinsi gani tunaweza kujenga maisha yetu juu ya Yesu Kristo?

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Wasaidie watoto wako wadogo kupata kitu fulani wanachofikiri kwa kweli ni imara. Je, walipata nini? Fundisha kwamba tunaweza kuwa imara pamoja na Yesu Kristo.



Septemba 2–8

## Ushuhuda wa Kristo

KWA AJILI YA HELAMANI 7–12

Watu wengi katika maandiko walifundisha na kushuhudia juu ya Yesu Kristo (ona Helemani 8:16–20). Wewe pia unaweza kuanza kujenga ushuhuda wako kuhusu Yeye! Ushuhuda ni kitu fulani unachoamini au kujua ni cha kweli kuhusu Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Andika ushuhuda wako na kuwa na desturi ya kuushiriki na familia yako au marafiki.

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Waulize watoto wako kitu kimoja wanachopenda kuhusu Yesu Kristo. Kisha shiriki ushuhuda wako wa Mwokozi pamoja nao.

VIELEZO NA KATY DOCKRILL



Septemba 9–15

## Samweli Akipanda Ukuta

KWA AJILI YA HELAMANI 13–16

Samweli alikuwa nabii aliyefundisha kuhusu Yesu Kristo juu ya ukuta wa mji (ona Helemani 13:4). Nenda kwenye ukurasa wa 12 na fanya sanaa kukusaidia kuelezea hadithi ya Samweli.

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Washikilie watoto wako wakati wamesimama juu ya kiti na washiriki kile wanachojua kuhusu Yesu Kristo kama Samweli aliyofanya.



Septemba 16–22

## Mchezo wa Kukusanya

KWA AJILI YA 3 NEFI 1–7

Yesu Kristo aliahidi atawakusanya watoto Wake wote kwa sababu Yeye anampenda kila mtu na anawataka wawe na injili (ona 3 Nefi 5:24). Cheza mchezo kuhusu kukusanya. Wafanye wachezaji wasimame katika duara. Mtu mmoja katikati anasema ukweli kuhusu wao, kama rangi yao wanayoipenda. Kiuhalisa hiyo ni kweli kwa yeote kwenye mchezo, wote wanakuja katikati pia. Endelea mpaka kila mmoja amekusanyika katikati.

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Cheza kombolela na watoto wako wadogo. Wakumbatie kwa nguvu unapowapata. Zungumza kuhusu jinsi Yesu Kristo anavyoahidi Yeye atatukusanya bila kujali wapi tulipo.



Septemba 23–29

## Yesu ni Nuru

KWA AJILI YA 3 NEFI 8–11

Yesu Kristo ni “nuru na uzima wa ulimwengu” (3 Nephi 9:18). Angalia mawio au machweo pamoja na familia yako. Kisha chora picha ya kile ulichokiona. Wakati unapochora, zungumza kuhusu sababu unazompendea Yesu Kristo na jinsi Yeye anavyokuletea nuru.

### Kwa ajili ya watoto wadogo :

Nenda nje na tazama nuru tofauti, kama juu, nyota au mwezi. Waulize watoto wako wadogo jinsi nuru inavyowafanya wahisi. Zungumza kuhusu jinsi Yesu Kristo ni nuru yetu.